# MORUWASA YETU

**MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MOROGORO**

**Toleo Maalum** | **Januari - Juni 2024**



## "VIONGOZI TUZUNGUMZE NA WANANCHI ULINZI WA MIUNDOMBINU YA MAJI"

### MHA. KUNDO MATHEW

*Uk....3*







**MORUWASA Habari na Matukio**

# UJUMBE WA MKURUGENZI MTENDAJI MORUWASA

Ninapenda kutumia nafasi hii kukukaribisha katika Jarida letu lijulikanalo kama MORUWASA YETU. Kupitia toleo hili ambalo ni la pili wadau na umma kwa ujumla utaweza kupata taarifa na uelewa kuhusu shughuli na matukio mbalimbali yaliyojiri katika Mamlaka kwa kipindi cha Januari 2024 hadi Juni 2024.



Katika kipindi hiki cha nusu ya mwaka wa fedha 2023/2024 Mamlaka imeweza kufanikisha majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha wananchi wa maeneo inayoyahudumia wanaendelea kupata huduma ya maji safi na salama ikiwa ni sambamba na kuendelea kuboresha huduma ya maji katika maeneo hayo.

Mamlaka imefanikisha zoezi la kufikisha huduma ya maji kwa wakazi wa Kiegea na Mkundi huku ikitarajia kuanza kuhudumia wananchi wa Lukobe kupitia mradi huo kuanzia Julai 2024. Sambamba na hilo Mamlaka imefanikisha kufikisha maji katika kitongoji cha Sokoine Ranchi, Dakawa. Maeneo haya hayajawahi kuwa na huduma ya majisafi.

Tunaendelea kupokea maombi ya maunganisho ya maji na nawasihi wateja na wananchi kuepuka kutumia vishoka katika kupata huduma za MORUWASA ili kuepuka hasara na usumbufu usio wa lazima.

Pamoja na kuendelea na utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira Mamlaka imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na uhujumu wa miundombinu ya maji kwa wizi wa maji na dira za maji; mivujo ya maji, maunganisho ya maji kinyume na utaratibu na malimbikizo ya bili zamaji , changamoto zote hizi zinarudisha nyuma jitihada za Mamlaka katika kutoa huduma bora na za viwango vya juu na zinaweza kukabiliwa na kumalizwa kwa ushirikiano wa karibu baina ya Mamlaka na wadau wetu.

Ndugu msomaji, tunapomaliza mwaka wa fedha 2023/2024 ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa wateja na wadau wote wa MORUWASA kwa mchango na ushirikiano mkubwa waliotuonesha katika kufanikisha utekelezaji wa kazi na majukumu ya Mamlaka. Ni dhahiri kwamba bila ya mchango wenu MORUWASA isingeweza kufanikisha majukumu yake kikamilifu.

Ni matumaini yetu kuwa tutaendelea kuwa mabalozi wazuri wa huduma zinazotolewa na MORUWASA na kuhakikisha tunaendelea kumtua mama ndoo kichwani kwa ufanisi mkubwa.

Mhandisi Tamim T. Katakweba
MKURUGENZI MTENDAJI

MORUWASA

# MHA. KUNDO: VIONGOZI TUZUNGUMZE NA WANANCHI ULINZI WA MIUNDOMBINU YA MAJI

Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Kundo Mathew, amewaomba viongozi wa Mkoa wa Morogoro wakiwemo viongozi wa Chama cha Mapinduzi mkoa wa Morogoro kuwasaidia kuzungumza na wananchi juu ya kulinda na kutunza miundombinu ya maji katika maeneo yao.



Mhe. Kundo ameyasema katika muendelezo wa ziara yake mkoani Morogoro wakati akikagua mradi wa kituo cha kusukuma maji kilichopo eneo la Kihonda Mizani ambapo moja ya changamoto inayoonekana katika maeneo mbalimbali ya Morogoro ni baadhi ya wananchi wasio na nia njema na wizara kuhujumu miundombinu ya maji.


Aidha Mhe. Kundo kwa niaba ya waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso ametoa maelekezo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA Mha. Tamim Katakweba kufanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha hadi kufikia mwishoni mwa mwezi juni 2024 anakamilisha matengenezo ya miundombinu ya Kituo hicho kufuatia athari za mafuriko yaliyotokea mwanzoni mwa mwaka huu ambapo mafuriko hayo yalisababisha hasara ya zaidi ya milioni 100 ambazo zilitumika kwa matengenezo ya pampu zote mbili, control panel ya transifoma na ujenzi wa sehemu ya ukuta ulioathirika na mafuliko hayo

Sambamba na kutembelea kituo cha kusukuma maji pia Mhe. Kundo ametembelea mradi wa tanki la maji Mgulu wa Ndege na kuhimiza uharakishwaji wa mradi kuanza kuhudumia kuhudumia wananchi wa Mkundi hukuakisisitiza maunganisho ya maji kufanyika ndani ya siku saba

Mhe. Mhandisi Kundo amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha kiasi cha Tsh. bilioni 1.4 za kutekeleza mradi wa Kituo cha Kusukuma Maji cha Mizani na Tsh. Bilioni 2.2 za kusambaza bomba katika mtandao wa usambazaji wenye urefu wa Km 250 katika maeneo ya Kihonda, Mkundi na Lukobe.

Mradi wa Kituo cha kusukuma maji cha Mizani ni mradi muhimu utakaokuwa na uwezo wa kuhudumia wananchi wapatao 135,000 wa kata za Kihonda, Lukobe na Mkundi.





# RAS MORO AIPA HEKO MORUWASA UTEKELEZAJI MRADI WA MGULU WA NDEGE

## ● MKUNDI MJIANDAE KWA MAUNGANISHO YA MAJI MAJUMBANI

**Morogoro, Juni 12,2024**

Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro Alhaj Ndg. Mussa Ali Mussa ameipongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) kwa utekelezaji wa mradi wa Mgulu wa ndege uliopo kata ya Mkundi Manispaa ya Morogoro.

Ametoa pongezi hizo wakati wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa wa Morogoro iliyoifanyika 12/06/2024 kwa lengo la kukagua maendeleo ya miradi mbalimbali mkoani Morogoro.

Aidha Alhaj Ndg. Mussa amemuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA kuhakikisha jitihada za haraka zinafanyika ili kukamilisha maunganisho ya maji kwa wananchi mapema ili kuondoa tatizo la maji katika kata ya Mkundi.

Katika hatua nyingine Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA, Ndg. Lyang'onjo Kiguhe ametoa ofa ya maji bure kwa siku tatu katika kizimba kilichopo maeneo ya Mkunsi Kwalung'waa na kuwaomba wananchi wa Mkundi kujiandaa na zoezi la maunganisho ya maji majumbani.

Kwa upande wake Mhe. Bi. Rebeca Nsemwa Mkuu wa Wilaya ya Morogoro ampongeza Mkurugenzi wa MORUWASA kwa kutoa ofa ya maji bure kwa muda siku tatu katika kizimba cha kwalung'waa na kuwahasa wakazi wa Mkundi kulinda miundombinu ya maji ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan.

Akisoma taarifa ya utekelezaji wa mradi huo Kaimu Meneja wa Maendeleo ya miundombinu MORUWASA,Mha.Harma Luwinzo amesema kuwa hadi sasa mradi mefikia 98% ya utekelezaji ambapo vipengele vilivyobaki ni ujenzi wa uzio kwa ajili ya usalama na choo cha mlinzi.

Mradi wa Tanki la maji la Mgulu wa ndege lina uwezo wa kubeba lita milioni mbili na litahudumia wananchi wa kata ya Mkundi na Lukobe huku tanki la Mlima Magereza lenye

# WANANCHI SOKOINE RANCHI WAANZA KUPATA MAJI

- MHA. KUNDO AWEKA JIWE LA MSINGI
- WANANCHI WAPONGEZA JUHUDI ZA SERIKALI



Hatimaye wananchi wa Kitongoji cha Sokoine Ranchi wameanza kupata huduma ya maji baada ya mradi wa maji ulioibuliwa na Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso kuanza kufikisha huduma kwa wananchi wa kitongoji hicho.

Akizungumza mara baada ya kuweka jiwe la msingi katika mradi huo naibu waziri wa maji Mhe. Mhandisi Kundo Mathew amemshukuru Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendeleakutekeleza azma yake ya kumtuma mama ndoo kichwani kwa vitendo.

Pia Mhe. Kundo amemshukuru amewapongeza viongozi wa Mvomero akiwemo Mbunge wa jimbo hilo Mhe. Zeeland na Mkuu wa wilaya ya Mvomero Mhe. Judith Nguli kwa jitihada na usimamizi wao wa kuhakikisha mradi wa Sokoine unatekelezwa kwa matokeo.

Katika hatua nyingine Mhe Kundo ametoa maelekezo kwa MORUWASA kukamilisha vituo vingine 11 vya kuchotea maji ifikapo mwishoni mwa mwezi Juni 2024.

Pia amewashukuru wananchi wa kitongoji hicho kwa ushirikiano mkubwa walioonesha kwa Serikali na kusisitiza kuwa ni marufuku wananchi kutumia maji pamoja na mifugo na wizara ya maji ipo kwa ajili ya kuhakikisha hilo linafanyika

Kwa upande wao wananchi wa kitongoji hicho wameeleza wazi furaha yao ya kupata maji huku wakiishukuru Serikaliya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia huduma ya majisafi na salama.

Mradi wa majisafi Sokoine Ranchi kata ya Dakawa wilayani Mvomero uliibuliwa Mhe Jumaa. Aweso Waziri wa Maji mnamo januari 2023 baada ya kubaini kuwa wananchi wa eneo hilo wanatumia maji ya kwenye mad-imbwi pamoja na mifugo ambapo aliagiza Mfuko wa Maji kutoa fedha za dharura ili kuhakikisha wananchi hao wanapata maji haraka iwezekenavyo.





# MHA. KUNDO : NAWAPONGEZA WATUMISHI WOTE SEKTA YA MAJI KWA BIDII YENU



Naibu waziri Wizara ya Maji Mhe Mhandisi Kundo Mathew amewapongeza watumishi wa sekta ya maji mkoani Morogoro kwa kufanya kazi kwa bidii na kuifanya sekta hiyo kuwa ni msaada wa upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wa mkoa wa Morogoro.

Ameyasema hayo katika kikao baina yake na watumishi wa sekta ya maji mkoa wa Morogoro kilichofanyika 25/05/2024 katika ukumbi wa hoteli ya Morena.

Mhe. Kundo amewaasa watumishi kupendana na kutojihusisha na majungu katika kazi kwani vitendo hivyo vinashusha ufanisi wa kazi katika Wizara.

Pia amewasisitiza watumishi wa sekta hiyo kufanya kazi kwa kushirikiana kwani mafanikio ya sekta ya maji hayaletwi na mtu mmoja

Pamoja na hayo Mhe. Kundo amewashukuru watumishi wa sekta ya maji kwa kumpokea vizuri katika wizara hiyo na kuahidi ushirikiano wa hali na mali katika kuhakikisha wizara ya maji inakuwa ni mfano bora kiutendaji katika utoaji huduma bora kwa wananchi wa Tanzania.

Ikumbukwe kuwa siyo muda mrefu tangu Mha. Kundo ateuliwe na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Naibu Waziri wa Maji chini ya waziri wake Mhe. Jumaa Aweso.

Kikao hicho kilihusisha watumishi walio chini ya sekta ya maji katika mkoa wa Morogoro kutoka taasisi za MORUWASA, BODI YA MAJI-BONDE LA WAMI RUVU,



# DC NSEMWA AONGOZA MAPOKEZI YA MTAMBO MPYA WA UCHIMBAJI 'EXCAVATOR' MORUWASA



Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Bi. Rebeca Nsemwa Februari 28,2024 ameongoza hafla ya mapokezi ya Mtambo wa uchimbaji 'Excavator' iliyofanyika katika ofisi za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA),ambapo utaiwezesha kutekeleza shughuli mbalimbali za Mamlaka hasa za matengenezo ya miundombinu ya Maji.



Mtambo huo wenye thamani ya takribani Tsh. Milioni 156 umenunuliwa kupitia Mradi Mkubwa wa Uboreshaji Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro unaofadhiliwa na Serikali kupitia Mkopo wa masharti nafuu.

Akiongea wakati wa hafla hiyo Mhe. Nsemwa amesema kuwa anaamini kuwa baada ya Mradi kero ya maji katika Manispaa ya Morogoro inaenda kutatuliwa na kuwasisitiza watumishi wa MORUWASA kuutunza mtambo huo.

Aidha Mhe. Nsemwa amewapongeza watumishi wa MORUWASA kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhudumia wananchi licha ya uwepo wa changamoto mbalimbali kwani anaamini kuwa Mradi huo unaenda kuboresha huduma ya maji na kutatua kero ya maji katika Manispaa ya Morogoro.

Kwa upande wake Mbunge wa Morogoro Mjini Mhe. Abdulaziz Abood ameipongeza MORUWASA kwa kununua Mtambo huo kwani unaleta matumaini ya kuwa Mradi umeanza kuleta matunda.

Hafla hiyo imehudhuriwa na Mwenyekiti Msaidizi wa Bodi ya Wakurugenzi MORUWASA, Menejimenti na Watumishi wa MORUWASA.



# RAS MOROGORO AMBANA MKANDARASI MRADI WA MAJI MIKUMI

Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro Ndg. Mussa Ali Musa amemtaka Mkandarasi Kampuni ya HelpDesk Engineering Tanzania Ltd anayetekeleza ujenzi wa Mradi wa Uboreshaji huduma ya Maji Mikumi kukamilisha na Kukabidhi Mradi huo ifikapo Mei 31,2024.



Ametoa maelekezo hayo leo Januari 15, 2024 wakati wa kikao baina yake, MORUWASA na Mkandarasi huyo kilichofanyika katika Ofisi za Mkuu wa Mkoa Morogoro kumsisitiza Mkandarasi kuwa hakutakuwa na nyongeza ya muda wa utekelezaji wa Mradi ambao awali h ulitakiwa kukamilika Novemba 2023.

Kwa upande wake Ndg. Suresh Kandhasamy ambaye ni Msimamizi wa Mradi kutoka HelpDesk Engineering Tanzania limited ameahidi kutekeleza maelekezo hayo ya kuhakikisha anatekeleza kazi zilizobaki katika ujenzi wa Mradi na Kuukabidhi ifikapo Mei 31,2024.

Mradi wa Uboreshaji Huduma ya Maji Mikumi unatekelezwa kwa fedha za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Maji kwa gharama ya takribani Tsh. Bilioni 3.18 chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) ambapo mnamo 12.01.2024 MORUWASA ilipokea Kiasi cha Shilingi Bilioni 1.2 za kuendelea kutekeleza ujenzi wa Mradi huu ambao hadi sasa umefikia asilimia

# MORUWASA YAKABIDHI ENEO LA UJENZI MRADI

- **UBORESHAJI HUDUMA YA MAJI MINDU**



Katika kutekeleza mradi wa uboreshaji huduma ya maji Mindu, MORUWASA imemkabidhi Mkandarasi Kampuni ya Greatain (T) Limited eneo la Mradi kwa ajili ya ujenzi wa Tanki lenye ujazo wa lita 500,000 na mtandao wa usambazaji maji kwa gharama ya takriban Tsh. 862,324,938 kwa ufadhili wa Serikali kupitia Wizara ya Maji.

Viongozi wa mitaa itakayonufaika na Mradi huo wamefurahia hatua hii ya kuanza kutekeleza mradi na kuahidi kutoa ushirikiano kwa Mkandarasi na Mamlaka.

Kukamilika kwa Mradi wa Maji Mindu kutanufaisha wananchi takariban 9,334 wa Mitaa ya Mindu, Mikoroshini, Mkwajuni na Madaganya Kata ya Mindu.

# KIKAO CHA BARAZA LA WAFANYAKAZI MORUWASA



Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) imefanya kikao cha Baraza la wafanyakazi Januari 30, 2024 ambacho kimeongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA Mha. Tamim Katakweba katika ukumbi wa Hoteli ya Kingsway Morogoro Mjini.



Wajumbe wa Baraza wamepata fursa ya kujadili masuala mbalimbali ya kiutumishi kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji kazi wa watumishi ili kufikia

Pia Baraza kupitia wajumbe limepitia na kujadili maoteo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Baraza la Wafanyakazi ni Baraza ambalo lipo kwa mujibu wa Agizo la Rais Na. 1 la mwaka 1970 kwa lengo la kuwashirikisha wafanyakazi wa ngazi zote katika utekelezaji wa shughuli za Taasisi kwa kushirikiana na Uongozi.



# MORUWASA WASHIRIKI KONGAMANO LA KISAYANSI LA MAJI



Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) imeshiriki katika Kongamano la tatu la Kimataifa la Kisayansi la Maji lililofanyika katika ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam.

Kongamano hilo lililoshirikisha Taasisi na Wadau mbalimbali wa Sekta ya Maji limefanyika sambamba na maadhimisho ya Miaka 50 ya Chuo cha Maji kauli mbiu ikiwa ni "Maji na Usafi wa Mazingira katika Ulimwengu unaobadilika".

Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Prof. Jamal Katundu akihitimisha Kongamano hilo Februari 02, 2024 amezipongeza Taasisi na wadau walizoshiriki na kuwataka kuongeza ushirikiano zaidi.


Pia amebainisha kuwa sera ya Taifa ya Maji inafanyiwa maboresho ili kuendana na mabadiliko mbalimbali ikiwa ni pamoja na ushirikishwaji wa Sekta binafsi.




*Bi. Neema Nyangi (kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma MORUWASA akipokea cheti cha shukrani kwaniaba ya MORUWASA kwa kudhamini kongamano la kimataifa la Maji kutoka kwa aliyekuwa katibu mkuu wizara ya Maji Prof. Jamal Katundu Februari 02,2024*

# MORUWASA YAPONGEZWA KUKIDHI VIWANGO VYA UBORA WA MAJI





Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) imepongezwa naTaasisi ya SPIN PISCINAS kutoka nchini Mexico kwa kuzingatia viwango vya ubora katika kutibu maji kabla ya kuyapeleka kwa Wananchi.

Pongezi hizo zimetolewa na Ndg. Hector Abaron Lance kwa niaba ya Taasisi hiyo mara baada ya kufanya vipimo vya sampuli ya maji katika mtambo wa kutibu na kusafisha maji wa Mambogo na kusema kuwa MORUWASA ni moja ya Taasisi za maji nchini inayozingatia ubora wa maji kabla hayajawafikia watumiaji.

Taasisi ya SPIN PISCINAS ipo nchini Tanzania ikitoa mafunzo ya namna bora ya kutibu maji na kuyafanya kukidhi viwango vya kuwa safi na salama kwa kutumia tekinolojia mpya na ya kisasa inayoitwa PROVITAB 3.





# MORUWASA YATOA ELIMU YA MAUNGANISHO YA MAJI KIHONDA



Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) imetekeleza maelekezo ya Mhe Mkuu wa Mkoa Mororogo Mhe. Adam Malima kuhusu kukutana na kutoa elimu ya maunganisho ya maji kwa viongozi wa Kata ya Kihonda kufuatia utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji Huduma ya Maji katika Kata za Kihonda, Lukobe na Mkundi ambao umeanza kunufaisha wananchi katika Kata ya Kihonda.

Elimu hiyo imetolewa Januari 09,2024 katika kikao kilichoongozwa na Mhe. Diwani Kata ya Kihonda Mhe. Hamisi Kilongo ilijikita katika utaratibu na gharama za maunganisho ya maji kwa ujumla.

Akitoa elimu hiyo Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano MORUWASA Bi. Neema Nyangi ameeleza kuwa ada ya maunganisho ya maji ni Tsh. 26,000 ambapo mwananchi atawajibika kugharamia vifaa vya maunganisho na uchimbaji wa mtaro kwa kuzingatia viwango atakavyopewa na wataalam wa Mamlaka.

Pia amewashukuru viongozi hao kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kuutoa kwa Mamlaka tangu kuanza kwa Mradi na kuwaomba kuendelea kushirikiana na Mamlaka katika hatua hii ya maunganisho ya maji.

Sambamba na hilo amewaomba viongozi hao kuendelea kuhamasisha suala la ulinzi wa Mradi

na kuepuka vitendo vya wizi wa Maji na uhujumu wa miundombinu ya maji ili huduma ya maji iweze kuwa endelevu na kuleta maendeleo kwa wananchi. Pia Mhe. Kilongo ametoa shukrani na pongezi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA kwa kazi kubwa iliyofanyika katika utekelezaji wa Mradi huu unaoenda kupunguza adha ya maji kwa wananchi wa Kihonda.

Kwa upande wao wenyeviti wa Mitaa wameipongeza MORUWASA na kuahidi kuendelea kutoa ushirikiano kwa Mamlaka katika hatua ya maunganisho ya maji.





## 08 MACHI, 2024

# SIKU YA WANAWAKE DUNIANI



Watumishi wanawake wa MORUWASA wameungana na wanawake wengine duniani katika kusherehekea kilele cha maadhimisho ya siku ya wanawake Duniani yaliyofanyika kimkoa katika Uwanja wa Shule ya Msingi Kiwanja cha Ndege, Manispaa ya Morogoro. Akizungumza kama mgeni rasmi wa maadhimisho hayo Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Adam Malima amepongeza wanawake wa Mkoa huo kwa jitihada na mchango wao mkubwa katika kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya mkoa wa Morogoro kupitia shughuli mbalimbali wanazozifanya.




"..niwapongeze akina mama wote wa Morogoro kwa kazi na jitihada mnazofanya za kuendeleza maendeleo ya mkoa wetu" amesema Mhe. Malima

Kwa upande wao wanawake wa MORUWASA kwa nyakati tofauti wameweka bayana furaha yao ya kushiriki katika maadhimisho hayo kwani yanawaongezea hamasa katika kutekeleza majukumu yao ya kumtua mama ndoo Kichwani na kuchochea maendeleo katika jamii na taifa kwa ujumla.

Kauli mbiu ya maadhimisho hayo kwa mwaka huu umebebwa na ujumbe "Wekeza kwa Wanawake, Kuharakisha maendeleo ya Taifa na Ustawi wa Jamii"

# MORUWASA YASHIRIKIANA NA WADAU KUPANDA MITI MOROGORO




Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) tarehe 04/06/2024, imeshirikiana na Manispaa ya Morogoro pamoja na wadau mbali mbali wa mazingira katika zoezi la kupanda miti lilifanyika katika shule ya sekondari Konga iliyopo kata ya Mzinga Manispaa ya Morogoro.

Zoezi hilo limefanyika ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya wiki ya mazingira ambacho kilele chake kitaifa kitafanyika Juni, 5, 2024 jijini Dodoma na mgeni rasmi atakuwa makamo wa Rais Mhe. Philip Mpango.

Rebeca Nsemwa ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Morogoro amezungumza wakati wa zoezi hilo amesema "niwaombe wananchi ambao mnapewa dhamana ya kupandiwa miti leo hii, tuwatie nguvu wadau wetu wa mazingira kwakuhakikisha miti tuliyopanda leo ina kuwa nakuleta tija kwa wananchi wa Morogoro na Tanzania kwa ujumla"

Aidha mtaalam wa Mazingira kutoka MORUWASA, Mha. Festo Mwandenene amewaomba wadau wa mazingira kuendelea kushirikiana na MORUWASA katika kutunza na kuendeleza miti iliyopandwa ili kuendelea kutunza vyanzo vya maji. kwa manufaa ya sasa na baadae katika upatikanaji wa majisafi kwa uhakika Mkoani Morogoro.

Maadhimisho ya wiki ya mazingira kwa mwaka huu yamebebwa na kauli mbiu " Urejeshwaji wa Ardhi iliyoharibiwa, na Usta-



KAMPENI UHIFADHI WA MAZINGIRA......

# MORUWASA, WAMI-RUVU,RUWASA,TARURA, TANROAD NA TANESCO ZAUNGANA

Taasisi sita Mkoani Morogoro zimeungana kuwa mstari wa mbele katika kuunga mkono kampeni maalumu ya uhifadhi wa Mazingira kwa Mkoa wa Morogoro iliyoanzishwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mhe. Adam Malima.

Viongozi wa Taasisi hizo ambazo zinahusisha MORUWASA, Bonde la Wami Ruvu, RUWASA, TANROAD,TARURA na TANESCO kwa pamoja wamemuahidi Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro Alhaji mhe. Mussa Ali Mussa kuhusu utayari wao wa kushiriki kikamilifu katika kampeni hiyo muhimu kupitia kikao kilichofanyika leo katika Ofisi ya Katibu Tawala

Akiongea kwa niaba ya Taasisi hizo Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA Mhandisi



Tamim Katakweba amesema kwa hatua hii ya awali Taasisi hizo kwa pamoja zitachangia jumla ya miche 6,000 kuunga mkono kampeni hiyo.

Naye Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro amezipongeza Taasisi hizo na kutoa msisitizo wa umuhimu wa Taasisi hizo kuwa mstari wa mbele katika kuhifadhi na kuzitaka kuendelea kuweka suala la mazingira katika programu zao za kitaasisi.

Kampeni hii ya uhifadhi wa Mazingira inalenga kuhifadhi Mazingira na vyanzo vya maji kwa kurejesha uoto wa asili kwa kupanda miche ya mazao mbadala ikiwemo Mikarafuu, Mikakao, michikichi na Miparachihi katika maeneo mbalimbali yaliyoathirika na uharibifu wa mazingira

# MORUWASA, SHANXI WASAINI MKATABA WA KUCHIMBA VISIMA VIREFU DAKAWA



Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) imesaini Mkataba wenye thamani ya Shilingi Bilioni 1.54 na Kampuni ya Shanxi Construction Engineering and Mineral Company kwa ajili ya uchimbaji wa Visima virefu Dakawa.

Shughuli ya uchimbaji wa visima hivi inaenda kufanyika kwa lengo la kujiridhisha kuhusu upatikanaji wa Maji ya kutosha katika eneo hilo ambapo yatatumika kama chanzo mbadala kwa wakazi wa Dakawa na Manispaa ya Morogoro.

Visima hivi vyenye urefu wa takriban mita 300 vitakuwa visima vya kwanza kwa ukubwa mkoani Morogoro.

Kwa mujibu wa Mkataba shughuli ya uchimbaji wa visima hivyo itatekelezwa ndani ya siku 90 kuanzia Leo ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro unaofadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Mkopo wenye masharti nafuu kutoka Shirika la Maendeleo la Ufaransa 'AFD'.

# MORUWASA YAIBUKA NA TUZO UTOAJI WA TAARIFA KWA WANANCHI



*Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Nnauye akimkabidhi tuzo Bi. Neema Nyangi (kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma MORUWASA*

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) imekabidhiwa tuzo kwa kufanya vizuri katika utoaji wa habari na taarifa kwa wananchi baada ya kuibuka mshindi wa 3 kati ya Mamlaka za maji 84 nchini.

Msemaji Mkuu wa Serikali Ndg. Thomas Makoba amesoma taarifa ya Vitengo vya Habari serikalini na Taasisi zilizofanya vizuri vitengo vya habari serikalini mapema leo mbele ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan ambaye alikuwa mgeni rasmi katika Kongamano la Pili la Maendeleo ya Sekta ya Habari nchini lililoambatana na kikao kazi cha 19 cha Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano Serikalini kilichofanyika katika ukumbi wa Mlimani City Dar es Salaam.

Tuzo hizo zilikabadhiwa na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Nnauye wakati wa kuhitimisha kikao kazi hicho tarehe 21 Juni,2024.

# MHANDISI AGAPITI M. JOSEPH MFANYAKAZI KINARA MORUWASA 2023/2024

- **Usimamizi thabiti wa Miradi**
- **Uwajibikaji na bidii katika kazi**
- **Kufanya kazi kwa Ufanisi**
- **Huduma bora kwa wateja**
- **Uadilifu**



## MWENGE WA UHURU 2024 WATEMBELEA MIRADI YA MAJI MAGADU NA KAUZENI



Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA Mha. Tamim Katakweba akisoma taarifa ya Mradi wa Maji wa Magadu mbele ya Kiongozi wa mbio za mwenge wa uhuru Bw. Godfrey Mnzava 22 Aprili, 2024.



Kiongozi wa mbio za mwenge wa uhuru Bw. Godfrey Mnzava akifungua bomba la maji katika mradi wa maji Kauzeni mara baada ya kukaguana kuridhishwa na uendelevu wa mradi



Mwenyekiti wa CCM wilaya ya Morogoro Ndg. Fikiri Juma akipokea taarifa ya mradi wa maji Kihonda kutoka kwa Meneja Uzalishaji maji na usambazaji maji MORUWASA Mha. Hafidh Lacha Katika ziara ya kamati ya siasa ya wilaya 13 Juni 2024



Naibu waziri wa wizara ya Maji Mhe. Mha. Kundo Mathew akiweka jiwe la msingi katika mradi wa majisafi Sokoine Lanch katika ziara yake mkoani Morogoro 26 May 2024



Baadhi ya watumishi wa MORUWASA wakiwa katika kikao na naibu waziri wa wizara ya maji Mhe. mha. Kundo Mathew kilichofanyika kwenye ukumbi wa Morena Morogoro 25 May 2024



Baadhi ya watumishi wa MORUWASA kwenye kikao maalum cha TUGHE kilichofanyika katika viwanja vya MORUWASA 28 Juni 2024

# MRADI WA MAJI KIHONDA WAANZA KULETA MATUNDA KWA WAKAZI WA KATA YA MKUNDI NA LUKOBE

















# PROF. KABUDI AZINDUA RASMI MASHINDANO YA RAMADHAN CUP 2024 KILOSA

- LENGO KUTOA ELIMU YA MAJI KWA JAMII
- ASISITIZA UTUNZAJI WA VYANZO VYA MAJI

Mbunge wa Jimbo la Kilosa Mhe. Prof Palamagamba Kabudi amezindua Rasmi Mashindano ya Mpira wa Miguu ya MORUWASA Ramadan Cup 2024 yenye lengo la kuiunganisha jamii kwa pamoja kutunza miundombinu na vyanzo vya maji sambamba na kuzingatia matumizi sahihi ya maji ambayo yalibebwa na ujumbe unaosema maji ni uhai tunza mazingira na vyanzo vya maji.



Akizungumza wakati wa kufunga rasmi michuano hiyo Mhe Prof. Kabudi aliwapongeza MORUWASA Kwa kuandaa mashindano hayo huku akisisitiza umuhimu wa wananchi kutunza vyanzo vya Maji na kulinda miundombinu ya Maji pamoja na kutokuharibu miundombinu ya umeme kwa kuwa inarudisha nyuma maendeleo kutokana na kukatikakatika kwa umeme ili kupisha matengenezo.

Mashindano ya Ramadan Cup ambato yameandaliwa na MORUWASA kanda ya Kilosa huku yakihusisha timu 12 za Wilaya ya Kilosa.

## MORUWASA FC YAICHAKAZA ABOOD MEDIA FC BAO 3 - 0

Timu ya mpira wa miguu MORUWASA FC imeibuka na ushindi wa mabao 3 - 0 dhidi ya Abood media FC katika mchezo wankirafiki uliopigwa katika uwanja wa ujenzi Morogoro.

MORUWASA FC ilijipatia goli la kwanza baada ya mlinzi wa Abood media fc kujifunga huku magoli mengine mawili yakipachikwa na Temba na Eliya Mwakajangwa.

Kwa ushindi huo timu ya MORUWASA FC imejinyakulia zawadi ya mbuzi

.Mechi hiyo ya kirafiki 11 Mei, 2024 ililenga kuhamasisha jamii juu ya utunzaji wa vyanzo vya maji kwa sambamba na kupiga vita vitendo vya uhujumu huduma za maji.



## NETBALL MORUWASA YAZIDI KUONESHA MAKALI

- Yailaza Ujenzi 8 - 3

Timu ya wasichana ya mpira wa pete MORUWASA imeibuka na ushindi wa 8-3 dhidi ya timu ya ujenzi katika mchezo wa kirafiki uliopigwa 29 Mei, 2024 kwenye uwanja wa chuo cha ujenzi Morogoro.










MORUWASA
LIPA BILI YAKO YA MAJI KUPITIA SIMU YAKO YA MKONONI
Ni rahisi ukiwa na Airtel Money
airtel money
PIGA *150*60#
Chagua 4 Lipa Bili
Chagua 3 Malipo ya Serikali
Chagua 1 Ingiza kumbukumbu namba
Ingiza kiasi cha Pesa unachodaiwa
Ingiza namba ya siri kulipia
Kumbuka Kumbukumbu namba yako ya malipo ya bili haibadiliki
moruwasa X moruwasa2 0736737736 0800751011 Bure


MORUWASA
LIPA BILI YAKO YA MAJI KUPITIA SIMU YAKO YA MKONONI
Ni rahisi ukiwa na T - PESA
T-PESA
PIGA *150*71#
Chagua 4 Lipa Bili
Chagua 5 Malipo ya Serikali
Chagua 1 Ingiza namba ya Malipo
Weka namba ya Malipo
Ingiza kiasi
Kumbuka Kumbukumbu namba yako ya malipo ya bili haibadiliki
moruwasa X moruwasa2 moruwasamaji 0736737736 0800751011 Bure


MORUWASA
LIPA BILI YAKO YA MAJI KUPITIA SIMU YAKO YA MKONONI
Ni rahisi ukiwa na Tigo Pesa
tigo pesa
PIGA *150*01#
Chagua 4 Lipa Bili
Chagua 5 Malipo ya Serikali
Chagua 1 Ingiza kumbukumbu namba
Ingiza kiasi
Ingiza namba ya siri kukamilisha malipo
Kumbuka Kumbukumbu namba yako ya malipo ya bili haibadiliki
moruwasa X moruwasa2 moruwasamaji 0736737736 0800751011 Bure


MORUWASA
LIPA BILI YAKO YA MAJI KUPITIA SIMU YAKO YA MKONONI
Ni rahisi ukiwa na HaloPesa
halo pesa
PIGA *150*88#
Chagua 4 Lipa Bili
Chagua 5 Malipo ya Serikali
Chagua 1 Ingiza kumbukumbu namba
Ingiza kiasi
Weka namba ya siri na kamilisha malipo
Kumbuka Kumbukumbu namba yako ya malipo ya bili haibadiliki
moruwasa X moruwasa2 moruwasamaji 0736737736 0800751011 Bure


MORUWASA
LIPA BILI YAKO YA MAJI KUPITIA SIMU YAKO YA MKONONI
Ni rahisi ukiwa na M-PESA
m-pesa
PIGA *150*00#
Chagua 4 Lipa kwa M-Pesa
Chagua 5 Malipo ya Serikali
Chagua 1 Namba ya Malipo Ingiza kumbukumbu namba
Weka kiasi cha pesa unachodaiwa
Ingiza namba ya siri kulipia
Kumbuka Kumbukumbu namba yako ya malipo ya bili haibadiliki
moruwasa X moruwasa2 0736737736 0800751011 Bure


MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MOROGORO
(MORUWASA)
Wewe kwetu ni wa Thamani
Kwa taarifa kuhusu Bili yako
Kwa taarifa kuhusu huduma za Maji
Malalamiko
Kwa taarifa kuhusu Mvujo
TUPIGIE
0800751011
BURE
1:30 Asubuhi - 4:00 Usiku
Ndani ya siku za kazi
@moruwasa X @moruwasa2 0736737736 0800751011 (Bure)

Jarida hili la MORUWASA YETU
Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano
na Uhusiano kwa Umma MORUWASA
S . L . P 5376, Morogoro

moruwasa X moruwasa2 moruwasamaji 0736737736 0800751011 Bure